
*Na.Rainolf Liganga,*
*Nyandeo parish,*
*Morogoro Tz.*

# TAJI LA DHIHAKA.







***Copied by Philemon Kajomola***
***kilombero parish 06/04/2014,***
***using capella professional.***
****** 0756 424278*******

**2a. Taji la dhihaka (miba) walimvisha yesu, ikatililika (damu) tokea kichwani,**

**b. Ni dhihaka gani (hiyo) unayoifanya, taji la mateso (hilo) kumvika Bwana.**

**3a. Jina lako zuri (sana) la watu wa Mungu, kumbe ni jambazi (mwizi)huko mitaani**

**b. Mwanga nalo giza (ndugu) havichangamani, tujifunze nini (kwako) tutaiga nini.**

**4a.Midomoni mwako (wewe) wamtaja yesu,lakini matendo(yako)menginikinyume**

**b.Zaka unatoa (sawa) kanisani upo, kwa ushirikina (bado) mtu maarufu.**

**5a. Familia yako (ndugu) umeisaliti, ile nyumba ndogo (sasa) imekuwa kubwa,**

**b. Wazitafutia (hizo) dhambi misitari, kwenye biblia ( ili ) kuzihalalisha.**

**6a.Na wewe kijana (wewe) wajitaabisha, likumbuke neon (lake) la Mungu lasema,**

**b.Msiyachokoze (haya) mambo yamapenzi, kwani muda wake (bado) haujafikia.**

**7a.Maneno machafu(wewe)unayatamka,pombenamadawa(vyote)vinakuendesha,**

**b.Nguo za aibu (wewe) unajivalia, ndugu na wazazi (ona) wanaaibika.**

**8a.Naye mnyang'anyi (yule) pale msalabani, alijitambua (kuwa) yeye ni mdhambi,**

**b.Ndipo akaomba (sana) yesu nikumbuke,naye Bwana yesu (kweli) akamsamehe.**

**9a.Uzito wa mwili (wake) Bwana wetu yesu, ulishikiliwa (sana) nayo misumari,**

**b.Hebu fikiria (tena) ndugu tafakari, ni mateso gani (haya) sababu ya nini.**